

Asante kwa Kutuma Hati Zako za Usasishaji wa Mpango wa Medicaid

Mpendwa [recipient name]:

Asante kwa kuwasilisha hati zako za usasishaji wa mpango wa Medicaid! Tumepokea maelezo yako na timu yetu sasa inakagua hati ulizowasilishwa.

Baada ya kukamilisha ukaguzi wetu, utapokea Notisi ya Uamuzi kuhusu Manufaa.

Tungependa ujue kwamba utaratibu wa ukaguzi utachukua muda kukamilika. Huenda usipate habari zozote kwa sasa. Hakuna haja ya kuwasiliana na Idara ya Huduma za Binadamu (Department of Human Services) au HealthSource RI ili upate taarifa. Utaendelea kutumia bima yako, hadi utakapopata habari kutoka kwetu.

Unaweza kuangalia hali ya usasishaji wa mpango wako wa Medicaid ikiwa una akaunti ya mtandaoni katika www.healthyrhode.ri.gov au ikiwa unatumia programu ya simu ya mkononi ya HealthyRhode. Ingia katika akaunti yako. Maelezo ya "My Renewal Information" yataonyeshwa baada ya kuingia katika akaunti.

Kinachoweza Kufanyika Ikiwa Utachelewa Kuwasilisha Maelezo Yako

Ni muhimu ujue kwamba ukichelewa kuwasilisha hati zako za usasishaji baada ya tarehe iliyowekwa kwenye notisi yako ya manjano ya usasishaji wa mpango wa Medicaid, huenda umepokea (au unaweza kupokea hivi karibuni) Notisi ya Uamuzi kuhusu Manufaa inayosema kwamba hustahiki kushiriki katika mpango wa Medicaid. Tukibainisha kwamba unastahiki kushiriki katika mpango wa Medicaid baada ya kukamilisha ukaguzi wetu wa hati zako ulizochelewa kuwasilisha, utarejeshewa bima yako ya Medicaid.

Ili upate maelezo zaidi kuhusu chaguo za bima yako wakati tunakagua hati hizi ulizochelewa kuwasilisha, wasiliana na HealthSource RI (HSRI) kuanzia saa 8 a.m. hadi 6 p.m. siku za wiki kwa nambari 1-855-840-4774.

Asante tena kwa kuwasilisha maelezo yako.